**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# HOTUBA YA KAIMU WAZIRI, WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**MHESHIMIWA SHARRIF ALI SHARRIF (MBM)**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**IMEWASILISHWA BARAZA LA WAWAKILISHI.**
**ZANZIBAR**

**MEI,2026**

YALIYOMO


A. UTANGULIZI ............................................................................1
A.1. Mwenendo wa Biashara..................................................3
i. Hali ya Uchumi na Biashara Duniani. ...................................3
ii. Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi Nyengine Duniani. .........4
iii. Biashara Kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. .......................5
iv. Hali ya Chakula na Bei Katika Soko la Zanzibar..................6
A.2. Mwenendo wa Viwanda ..................................................6
A.3. Muundo na Majukumu ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ....................................................9
B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI.........................11
C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI,2026. ..........................................................12
i. Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ...............................................................12
ii. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 13
iii. Mafanikio ya Ukusanyaji wa Mapato...................................13
iv. Changamoto ya ukusanyaji wa Mapato ............................13
D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 ..................14
E. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026. .................18
PR0101: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. ..............19
PR0102: Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali ...................................................................24
PR0103: Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara.........................................................................27

F. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026....41
F.1. Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)....41
F.2. Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar (BPRA).....43
F.3. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)....45
F.4.Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO)....47
G. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE KWA IDARA NA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027....51
G.1. Vipaumbele vya Idara na Taasisi Zinazopokea Ruzuku kwa Mwaka 2026/2027....51
G.2.Sekta ya Viwanda....51
G.3. Sekta ya Biashara....52
G.4. Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma 52
H. VIPAUMBELE KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027....53
H.1. Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA)....53
H.2.Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)....54
H.3. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)....54
I. MWELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027....55
I.1. Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027....55
I.2. Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027....55
J. SHUKRANI:....58
K. HITIMISHO....59
L. VIAMBATANISHO....61
Kiambatanisho Nambari 1:....61
Kiambatanisho Nambari 2:....62
Kiambatanisho Nambari 3:....63

Kiambatanisho Nambari 4: ....................................................65
Kiambatanisho Nambari 5: ....................................................66
Kiambatanisho Nambari  6: ..................................................67

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa madhumuni ya kupokea, kupitia, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi yanayojumuisha Fungu 017 la Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kazi za kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** Kabla sijaanza hotuba hii naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika Baraza lako hili leo tukiwa wazima wa afya na kuendelea kutekeleza majukumu ya kujenga nchi yetu kwa usalama na ufanisi mkubwa katika kipindi hiki cha pili cha Awamu ya Nane ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa neema katika kuendeleza ujenzi wa Taifa na kuwaletea maendeleo wananchi wote kwa ujumla.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa uongozi wake mahiri na jitihada anazozichukua kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Sote ni mashahidi wa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo na kuonesha dira ya mwelekeo wa Taifa hususani katika kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo ambayo ina tija kwa wananchi. Nitumie fursa

hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu pamoja na wananchi wote kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa Rais wetu nguvu, ulinzi, afya njema na kila lililo la Kheri katika kuwatumikia Wazanzibari.

4. **Mheshimiwa Spika,** Pia nachukua fursa hii, kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** kwa kuendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka 2025-2030 pamoja na mipango yote ya maendeleo ikiongozwa na Dira ya Maendeleo ya 2050. Ni matarajio ya wananchi kwamba Ilani na Mipango hiyo itatekelezwa kwa ufanisi kutokana na jitihada anazochukua katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuleta maendeleo ya Taifa letu.

5. **Mheshimwa Spika**, Nachukua fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza katika kuliongoza Baraza hili na kwa maelekezo wanayotupa ambayo yanalenga kuimarisha utendaji kazi. Ni matumaini yetu kwamba uongozi wenu utaliwezesha Baraza hili kutekeleza majukumu yake kwa weledi na maarifa makubwa.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ambayo ni Kamati ya kudumu ya Baraza chini ya uongozi wa Mheshimiwa Fatma Ramadhan Mohammed, Mwakilishi wa Wanawake Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti,

Mheshimiwa Dkt. Mohammed Ali Suleiman, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mtambwe na Wajumbe wote wa Kamati kwa michango, ushauri, mashirikiano na miongozo wanayotupatia wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya bajeti hii yamezingatia miongozo mbali mbali iliyowekwa na Serikali ikiwemo Mipango mikuu ya Kitaifa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025-2030, Maagizo ya Mheshimiwa Rais Wakati wa Uzinduzi wa Baraza la 11 la Wawakilishi na maagizo na ahadi alizotoa wakati wa Kampeni, Mpango Mkuu wa Maendeleo wa Zanzibar pamoja na Sera za Wizara.

8. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukrani na maelezo hayo ya awali, naomba kuanza Hotuba hii kwa kuwasilisha utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na hatimae kuwasilisha mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## A.1. Mwenendo wa Biashara

### i. Hali ya Uchumi na Biashara Duniani.

9. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Ripoti ya Biashara pamoja na Takwimu Duniani ya mwezi Machi, 2026 (Global Trade Outlook and Statistics March, 2026) inaonesha kuwa mwenendo wa Biashara Duniani umeongezeka kwa takribani asilimia 4.6 ikilinganishwa na mwaka 2025, ikichangiwa na kuongezeka kwa biashara ya bidhaa

zinazohusiana na Akili Mnemba, Tehama na uagizaji. Hata hivyo, ukuaji wa biashara unatarajiwa kupungua kwa kiasi kikubwa hadi kufikia asilimia 1.9 mwishoni mwa mwaka 2026, hii inatokana na kudhoofika kwa mahitaji ya kimataifa, kuongezeka kwa mivutano katika siasa za Kimataifa na bei ya juu ya nishati inayohusishwa na migogoro inayoendelea Duniani, ambapo bei za nishati zinatarajiwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mwaka 2025, biashara ya dunia katika uagizaji na usafirishaji wa bidhaa na huduma imekuwa ikilinganishwa na mwaka 2024, na kufikia dola trilioni 35, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7. Ukuaji huu umetokana na kuongezeka kwa biashara ya huduma na ongezeko la biashara kati ya nchi zinazoendelea.

**ii. Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi Nyengine Duniani.**

10. **Mheshimiwa Spika,** Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji wa bidhaa nje umepelekea hali ya biashara kwa ujumla kuimarika, ambapo kwa mwaka 2025 Zanzibar ilifanya biashara yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2,590.6 ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 1,825.5 kwa mwaka 2024 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 41.9. Bidhaa zilizosafirishwa kwenda nje ya Nchi ni pamoja na karafuu, vitenge, khanga, mwani, mazao ya baharini, vyuma chakavu, makapi ya ngano na ngozi za n'gombe na bidhaa zilizoagizwa ni pamoja na bidhaa za chakula, dawa na vipuri vya magari.

11. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 92.4 kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 105.28 mwaka 2024. Kiwango hicho cha usafirishaji kimepungua kwa asilimia 12.2 na hii imetokana na usafirishaji mdogo wa karafuu na bidhaa ya mwani. Bidhaa hizo zilisafirishwa katika masoko ya Cameroon, China, Kenya, Comoro, Mozambique,South Africa, Madagascar, Singapore, Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Indonesia, India na Denmark Bangladesh na Oman.

12. **Mheshimiwa Spik**a, Kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 2,498.18 kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1,649.26 kwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 51 ikilinganishwa na mwaka 2024. Bidhaa ambazo Zanzibar imeagiza kutoka nchi za nje ni pamoja na mafuta, bidhaa za Viwandani, vyombo vya usafiri, nguo na bidhaa za chakula. Bidhaa hizo zimetoka nchi za Falme za Kiarabu, China, India, Pakistani, Brazil, Uturuki na Vietnam.

**iii. Biashara Kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.**

13. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2025, Zanzibar ilisafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara zenye thamani ya Shilingi Bilioni 90.57 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 106.32 zilizosafirishwa mwaka 2024. Miongoni mwa bidhaa zilizosafirishwa kwenda Tanzania Bara ni pamoja na chuma chakavu,

mafuta ya kupikia, mchele wa basmati na bidhaa nyengine za vyakula vya makopo. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2025, Zanzibar iliagiza kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 400.64 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 382.51 kwa mwaka 2024. Miongoni mwa bidhaa hizo ni pamoja na mchele, mbatata na bidhaa za mbogamboga

#### iv. Hali ya Chakula na Bei Katika Soko la Zanzibar

14. **Mheshimiwa Spika,** Hali ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula hapa nchini inaendelea kuridhisha na vyakula vyote muhimu vinaendelea kupatikana bila ya usumbufu. Kwa upande wa bei za bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, unga wa ngano, sukari na mafuta ya kupikia katika masoko ya ndani zinaendelea kuwa tulivu. Hali hii imetokana na uwepo wa bidhaa hizo kwenye mzunguko pamoja na Wizara kusimamia hali ya ushindani halali wa bei katika soko. Aidha, uzalishaji wa unga wa ngano umeendelea kuimarika ambapo jumla ya Tani 63,281 za unga wa ngano zimezalishwa katika kiwanda cha Zanzibar Milling kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026. Na uzalishaji wa sukari katika Kiwanda cha Sukari Mahonda jumla ya tani 5,379 za sukari zimezalishwa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026.

### A.2. Mwenendo wa Viwanda

15. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya viwanda inaendelea kuwa muhimili muhimu wa uchumi wa Taifa. Kwa mwaka wa

fedha 2024/2025 mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa ulifikia asilimia 20.8. Aidha, kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2025 hadi Machi 2026 mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la Taifa umefikia asilimia 19.3. Matarajio ni kufikia zaidi ya asilimia 20 ifikapo mwezi Juni 2026.

16. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla sekta ya viwanda inaendelea kuimarika kutokana na ongezeko la uzalishaji viwandani pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati hasa katika sekta ya ujenzi, maji na umeme inayochochea shughuli za viwanda.

17. **Mheshimiwa Spika,** Ongezeko hili linatokana na kuanzishwa kwa viwanda vipya ambavyo ni Maisha bottler's Ltd kinachozalisha vinywaji baridi kilichopo Maruhubi, Ikraam bottler's and creamery Ltd kinachozalisha maji ya kunywa kilichopo Hanyegwa Mchana, Altu – Pet Food Manufacturing Company Ltd kinachozalisha chakula cha paka kilichopo Kiembe samaki, Mama Afrika kinachozalisha nguo kilichopo eneo la Viwanda Dunga Zuze na Flying Fox kinachozalisha unga wa ngano kilichopo Finya Mkoa wa Kaskazini Pemba. Vilevile, Wizara inaendelea na jitihada za kuhamasisha Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) katika maeneo ya viwanda Dunga Zuze. Katika jitihada hizo jumla ya Wawekezaji 22 wamejitokeza, kati ya hao Wawekezaji 12 wamepatiwa maeneo na tayari watano (5) wameshaanza ujenzi wa miradi katika Eneo la Viwanda Dunga ambao ni Reysion Enterprise Ltd, Africa

Bio Chem Co Ltd, Naf Traders Ltd, Arenist Group (z) Company Ltd na Eco Pro Company Ltd.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation (ZMCL) kimezalisha jumla ya tani 63,281 za unga wa ngano na tani 19,098 za pumba kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na tani 56,785 za unga wa ngano na tani 17,686 za pumba kwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 11.4 kwa unga wa ngano na asilimia 0.1 kwa pumba. Aidha, kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 213.

19. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Sukari Mahonda kimepanga kuzalisha tani 6,179 za sukari kwa mwaka 2025/2026, hadi kufikia mwezi wa Machi 2026 kimeweza kuzalisha tani 5,379 za sukari ikilinganishwa na mwaka 2024/2025 ambapo kiwanda kilipanga kuzalisha tani 9,000 za sukari, hadi kufikia Machi 2025, tani 7,900 za sukari zilizalishwa, kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 120.

20. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Drop of Zanzibar kimeweza kuzalisha lita 52,357,030 za maji ya kunywa kwa mwaka 2025/2026 ukilinganisha na lita 49,292,080 kwa mwaka 2024/2025 ongezeko hili ni sawa na asilimia 6.2, kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 85.

21. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zainab Bottlers kimeweza kuzalisha lita 30,350,055 za maji ya kunywa kwa mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na lita 24,431,896 kwa mwaka 2024/2025 ongezeko hili ni sawa na asilimia 24. Aidha kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 268.

22. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Viwanda vilivyotajwa hapo juu, Wizara inathamini juhudi zinazofanywa na Viwanda vyengine vidogo vyenye kuzalisha bidhaa za aina mbali mbali ikiwemo samani, vifungashio, uzalishaji wa chumvi, uchakataji wa matunda, mwani na viungo.

## A.3. Muundo na Majukumu ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imeundwa na Idara nne (4) ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Maendeleo ya Viwanda, na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na Afisi Kuu Pemba. Aidha, Wizara inasimamia Taasisi 10 zikiwemo Taasisi zinazopokea Ruzuku na Taasisi zinazojitegemea ambazo ni; Tume ya Ushindani Halali wa Biashara (ZFCC); Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara (BLRA); Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC); Baraza la Ushindani Halali wa Biashara (ZFCT); Wakala wa Vipimo (ZAWEMA); na Afisi ya Usajili wa Hakimiliki (COSOZA). Aidha, kwa upande wa Taasisi zinazojitegemea ni pamoja na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Wakala wa Usajili Biashara na Mali (BPRA), Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na Kampuni ya Mwani (ZASCO) ambayo kwa sasa imehamishiwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Wizara kwa ujumla inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:-

i. Kuandaa na kusimamia Mipango, Sera, na Tafiti zinazohusiana na Sekta zilizo chini ya Wizara;
ii. Kusimamia kuwepo kwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji;
iii. Kusimamia na kuimarisha mazingira mazuri ya ufanyaji Biashara;
iv. Kuhakikisha bidhaa na huduma zinazozalishwa na kuagizwa zinakidhi viwango vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
v. Kuhakikisha uwepo wa masoko ya Nje ya Nchi kwa bidhaa za ndani;
vi. Kusimamia na kukuza maendeleo ya Viwanda;
vii. Kusimamia shughuli za usajili wa biashara na mali;
viii. Kusimamia usawa wa Vipimo katika ushindani wa kibiashara;
ix. Kusimamia utoaji wa leseni ili kupunguza utitiri wa tozo na kurahisisha utoaji wa leseni na vibali;
x. Kusimamia maendeleo ya karafuu kwa kununua na kuuza karafuu nje ya nchi;
xi. Kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa zinazotokana na maamuzi ya Tume ya Ushindani Halali wa Biashara pamoja na mamlaka nyengine za udhibiti;
xii. Kuweka utaratibu wa majadiliano ya kibiashara baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; na
xiii. Kusajili, kukusanya na kugawa mirabaha kwa Wamiliki husika wa haki miliki waliosajiliwa.

## B.VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipanga kutekeleza Vipaumbele katika maeneo makuu matatu (3) ambayo yalilenga kuimarisha Sekta ya Viwanda, kuimarisha Sekta ya Biashara na kutafuta masoko pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara na utoaji wa huduma.

**25. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Sekta ya Viwanda, Wizara ilipanga kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda Dunga, Chamanangwe na Pangatupu ili kuweza kuvutia uwekezaji katika maeneo hayo. Aidha, katika kuimarisha biashara na utafutaji wa masoko Wizara ilipanga kuendeleza ujenzi wa Kituo cha maonesho ya biashara Dimani pamoja na kuratibu ujenzi wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano Fumba.

**26. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Taasisi zilizo chini yake inaendelea kuimarisha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma kwa kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Taasisi, kuimarisha mifumo ya Tehama kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuongeza usajili wa mali na biashara na kusimamia ubora wa bidhaa. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha wigo wa ununuzi wa karafuu pamoja na kutafuta masoko mapya ya mwani kwa wakulima.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI, 2026.

27. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inatekeleza majukumu yake kupitia Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni ZFCC, BLRA, ZNBC, ZFCT, ZAWEMA na COSOZA. Aidha, Wizara inasimamia utekelezaji wa taasisi zinazojitegemea ambazo zipo chini ya Wizara zikiwemo ZBS, BPRA, ZSTC na ZASCO.

### i. Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

28. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni 57.55 kwa ajili ya kutekeleza programu zake, kwa kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026, Wizara ilipanga kutumia jumla ya Shilingi Bilioni 55.12, hadi kufikia Machi 2026 Wizara imetumia jumla ya Shilingi Bilioni 19.55 ambayo ni sawa na asilimia 35 ya makadirio ya Julai 2025– Machi 2026.

29. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha zilizopatikana ni jumla ya Shilingi Bilioni 2.54 sawa na asilimia 13 ziliingizwa kwa ajili ya mishahara, Shilingi Bilioni 12.66 sawa na asilimia 65 ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo, Shilingi Bilioni 3.66 sawa na asilimia 19 ziliingizwa kwa matumizi ya Ruzuku na Shilingi Milioni 674.34 sawa na asilimia 3 ziliingizwa kwa kazi za kawaida. Mchanganuo wa matumizi hayo unaonekana katika **Kiambatanisho nambari 1 na 2.**

### ii. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

30. **Mheshimiwa Spik**a, Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 3.51 kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Wizara ilipanga kukusanya Shilingi Bilioni 2.82. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Shilingi Bilioni 1.26 zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia 45 ya makadirio ya makusanyo kwa miezi tisa (9). Mchanganuo wa mapato kwa ujumla unaonekana katika **Kiambatanisho Nambari 3.**

### iii. Mafanikio ya Ukusanyaji wa Mapato

31. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 Wizara kupitia Taasisi zake imefanikiwa kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuboresha mifumo ya usajili wa biashara na mali, kuongeza vituo vya usajili wa biashara eneo la Paje na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma katika soko la ndani.

### iv. Changamoto ya ukusanyaji wa Mapato

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inakabiliwa na mwitikio mdogo wa Taasisi zinazotoza Leseni na Tozo kwa kutokuwasilisha michango yao ya asilimia moja kwa Mamlaka ya Udhibiti ya Usimamizi wa utoaji wa Leseni. Aidha, ucheleweshaji wa Taasisi za Serikali katika

kuwasilisha malipo ya ukumbi wa mikutano katika eneo la maonesho Dimani na ukodishaji wa vifaa yamechangia upungufu wa ukusanyaji wa mapato, hadi sasa Wizara inazidai Taasisi hizo jumla ya Shilingi Milioni 455.67. Kwa sasa Wizara imechukua jitihada za kufuatilia madeni hayo sambamba na kuwaandikia barua za ukumbusho.

33. **Mheshimiwa Spika,** Mbali ya changamoto katika ukusanyaji wa mapato Wizara inakabiliwa na changamoto nyengine kama ifuatavyo:-

i. Kutopatikana kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati jambo ambalo linapelekea kutokukamilika kwa miradi kwa muda uliopangwa.
ii. Uhaba wa maeneo (Ofisi) ya kufanyia kazi pamoja na Ofisi ilizonazo kutokuwa katika mazingira mazuri hali ambao inaathiri mazingira ya kazi na Taswira za Taasisi.
iii. Wizara inakabiliwa na uhaba wa wataalamu katika kada za biashara na Viwanda, ukosefu wa vifaa muhimu vya kufanyia kazi ikiwemo vyombo vya usafiri na mifumo ya Tehama jambo ambalo linapelekea kushuka kwa ufanisi katika utendaji na kupelekea upungufu wa ukusanyaji wa mapato.

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia

programu zake imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo miwili ambayo ni Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza maeneo ya Viwanda (Industrial Parks) pamoja na mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar. Aidha, Wizara imesimamia utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango (ZBS) pamoja na Programu ya kuimarisha biashara na kuongeza ufanisi kwa kutumia falsafa ya Kaizen.

35. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipanga kutumia Shilingi Bilioni 46.31 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi Bilioni 35.56 kwa ajili ya Mradi wa Kuanzisha na kuendeleza maeneo ya Viwanda (Industrial Parks) na Shilingi Bilioni 10.80 kwa ajili ya mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. **Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo ya Viwanda (Industrial Parks)**

36. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuanzisha na kuendeleza maeneo Tengefu ya Viwanda kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kutengeneza bidhaa za viwandani, kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuongeza mauzo ya nje. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu ulipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 35.56. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) mradi ulipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 35.56 na hadi kufikia Machi 2026, mradi huu umeingiziwa jumla ya

Shilingi Bilioni 9.87 sawa na asilimia 28. Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imefanikiwa kuendeleza miundombinu ya ujenzi wa tangi la maji kwa kuchimba visima viwili vya maji pamoja na ujenzi wa chumba kitakachohifadhia genereta umeanza kwa hatua za msingi. Ujenzi huo umefikia asilimia 42.39 .

ii. Wizara imekamilisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika eneo la Viwanda Pangatupu. Eneo hilo lina ukubwa wa ekari 483.

iii. Wizara imefanikiwa kulipima na kuliwekea alama eneo la ziada la Viwanda Dunga Zuze ambapo jumla ya hekta 243 ikiwa ni nyongeza za hekta 62.8 za awali zimepatikana. Lengo la kuongeza eneo hilo ni kuweka mazingira bora ya Uwekezaji wa Viwanda. Aidha, Wawekezaji 22 wamejitokeza, kati ya hao Wawekezaji 12 wamepatiwa maeneo na tayari Wawekezaji watano (5) wameanza ujenzi wakiwemo Reysion Enterprise Ltd, Africa Bio Chem Co Ltd, Naf Traders Ltd, Arenist Group (z) Company Ltd na Eco Pro Company Ltd.

iv. Wizara imefanya ununuzi wa mitambo miwili (2) ya uzalishaji wa mbolea ya maji (liquid bio-stimulant) na uzalishaji wa mbolea ngumu na chakula cha mifugo ambayo inatarajiwa kufungwa katika kiwanda cha Mwani Chamanangwe.

**ii. Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar.**

37. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa kuweka eneo la kisasa kwa ajili ya maonesho. Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ilipanga kutumia jumla ya Shilingi Bilioni 10.80 kwa kipindi cha miezi tisa (9) mradi ulipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 10.80  Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Shilingi Bilioni 2.79 sawa na asilimia 26 zimetumika.

**iii. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)**

38. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZBS imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ZBS imeweza kukamilisha Ujenzi wa Maabara ya Metrolojia  pamoja na ununuzi wa vifaa vya Metrolojia kwa awamu ya  kwanza. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mradi huu ulipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 2.78. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Shilingi Milioni 756.48 zimetumika sawa na asilimia 27.24

**iv. Programu ya  Kuimarisha Biashara na Kuongeza Ufanisi kwa Kutumia Falsafa ya Kaizen**

39. **Mheshimwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kuimarisha biashara na kuongeza ufanisi kwa kutumia falsafa ya Kijapani ya Kaizen kupitia mradi wa ‘’The Project on Strengthening Enterprises through Business

Development Service (BDS) and quality and productivity improvement (Kaizen)" ambao unaendeshwa kwa mashirikiano kati ya Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

i. Wizara imetoa mafunzo ya Kaizen kwa wataalamu kutoka sekta ya Umma na Binafsi wakiwemo wakufunzi wa vyuo vikuu, wataalamu wa Taasisi za Serikali, pamoja na wataalamu kutoka kampuni mbali mbali zinazojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za viwandani.
ii. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Duniani (UNIDO), imetoa mafunzo ya Kaizen kwa wajasiriamali 60 wanaosarifu bidhaa za mwani Unguja na Pemba, ambapo wajasiriamali 7 kati yao wameendelea na mafunzo ya vitendo baada ya mafunzo ya darasani.
iii. Jumla ya wataalamu wanne (4) wameshiriki mafunzo ya muda mfupi nchini Japan yanayohusiana na program ya Kaizen kwa ajili ya kuongeza ujuzi.

## E. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI, 2026.

**40. Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda yanatekelezwa kupitia programu kuu tatu ambazo ni ;Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali na Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hizo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara za Wizara, Afisi Kuu Pemba pamoja na Taasisi zake ikiwemo ZFCC, BLRA, ZNBC, ZFCT, ZAWEMA na COSOZA ambapo utekelezaji wa programu hizo ni kama ifuatavyo:-

**PR0101: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.**

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kutoa huduma za Kiofisi kwa ufanisi na ustawi wa sekta ya Biashara na Viwanda. Programu hii imegawika katika Programu Ndogo tatu (3) kama ifuatavyo:-

i. Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara.
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 4.52 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Programu hii ilipangiwa Shilingi Bilioni 3.52 na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya Shilingi Bilioni 2.68 sawa na asilimia 76 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii. Mafanikio ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:-

**SR010101: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina jukumu la kusimamia Sheria na Kanuni za Kiutumishi pamoja na ustawi wa rasilimali watu. Mafanikio ya utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imefanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu na kuuwasilisha Afisi Kuu ya Utumishi kwa hatua zinazofuata.

ii. Wafanyakazi arobaini na nne (44) wamepatiwa likizo ya kawaida na kulipwa stahiki zao za likizo kwa mujibu wa miongozo. Vile vile, Wizara imeendelea kutoa fursa za mafunzo kwa wafanyakazi ishirini na tatu (23) ambapo wafanyakazi 15 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi wanane (8) wanaendelea na masomo ya muda mrefu katika kada mbali mbali.

iii. Wizara imesimamia manunuzi mbali mbali ya vitendea kazi, kulipia huduma za uendeshaji wa Ofisi.

iv. Wizara imeshiriki mikutano 21 ya majadiliano ikiwemo Mikutano ya Kimataifa nane (8), Kitaifa tisa (9), Kikanda nne (4).

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Ofisi ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 2.95 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 – Machi, 2026, Programu hii

ndogo ilipangiwa Shilingi Bilioni 2.32. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya Shilingi Bilioni 1.98 sawa na asilimia 86 zimeingizwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

**SR010102: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara**

**46. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kutoa huduma za uandaaji na uibuaji wa tafiti, uandaaji na utekelezaji wa Mipango pamoja na usimamizi wa takwimu za Wizara. Mafanikio ya utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imekamilisha uandaaji wa Sera ya Miliki Bunifu "Zanzibar Intellectual Property Policy 2026" na sasa ipo tayari kwa utekelezaji.
ii. Wizara imefanya mapitio ya utekelezaji wa ripoti ya Tathmini ya Mazingira ya Biashara (2025) kwa Taasisi na Wizara za Serikali kwa kuangalia maeneo ambayo yameshafanyiwa kazi katika kuondoa changamoto za ufanyaji biashara.
iii. Wizara imeandaa Rasimu ya Mkakati wa Mauzo ya Nje wa Zanzibar ambao umeonesha mwenendo na ukuaji wa mauzo ya nje ya nchi, changamoto na fursa zilizopo.
iv. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) imekamilisha zoezi la ukusanyaji maoni kwa wadau wa biashara kwa ajili ya uandaaji wa mradi wa Kuimarisha uwezo wa biashara na ushindani katika masoko ya Kikanda

na Kimataifa kwa kuzingatia sekta za biashara ya kilimo na uchumi wa buluu awamu ya III.

v. Wizara imefanya kikao cha uelewa wa ujazaji wa fomu za takwimu za biashara na Viwanda ambazo zitatumika katika kukamilisha Mkakati wa Maendeleo ya Takwimu Zanzibar (ZSDS) unaosimamiwa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

vi. Wizara imeandaa na kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Shughuli za Wizara na Miradi ya Maendeleo kwa vipindi vya robo mwaka na nusu mwaka katika Mamlaka husika.

vii. Wizara inaendelea na uandaaji wa Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (MICE).

47. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Milioni 482.52 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu hii ilipangiwa Shilingi Milioni 379.55 na hadi kufikia Machi, 2026. Jumla ya Shilingi Milioni 256.96 sawa na asilimia 68 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010103: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.**

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Mafanikio ya utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo: -

i. Jumla ya wafanyakazi sita (6) wamepatiwa mafunzo ambapo wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya pili na wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya Diploma. Aidha, Wizara imewapatia wafanyakazi tisa (9) likizo.
ii. Wizara imefanya vikao vitatu (3) vya kujenga uelewa juu ya Maadili ya watumishi pamoja na masuala mtambuka.
iii. Wizara imevitembelea Viwanda kwa ajili ya kusikiliza changamoto zao na kuwapatia ushauri wa kuendeleza sekta hii vikiwemo kiwanda cha WaterCom, Amos Industry, Flying Fox, Swahili Salt industry na Fair Sale.
iv. Wizara imefanya kikao kimoja (1) na wadau wa Viwanda kwa lengo la kuhamasisha umuhimu wa sekta ya viwanda.
v. Wizara imeratibu ushiriki wa wajasiriamali katika maonesho ambapo jumla ya Wajasiriamali wanne (4) wameshiriki katika maonesho ya saba saba Tanzania Bara, Wajasiriamali watatu (3) walishiriki katika maonesho ya nane nane Morogoro na Wajasiriamali watatu (3) walishiriki katika maonesho ya nane nane Kizimbani Unguja.
vi. Wizara imefanya vikao 3 na wadau wa sekta ya biashara ambapo viliangalia changamoto zinazotokana na uingizaji na usafirishaji wa bidhaa mbali mbali zikiwemo Mpira, Samaki, Pweza na bidhaa nyengine za mboga mboga.

49. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 1.08 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 programu hii ilipangiwa Shilingi Milioni 822.33. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya Shilingi Milioni 440.41 sawa na asilimia 54 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**PR0102: Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**

50. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda. Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji wa Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Programu hii ina jukumu la kuongeza mchango wa sekta ya uzalishaji Viwandani katika Pato la Taifa.

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 36.01 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Programu hii ilipangiwa Shilingi Bilioni 35.92 na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya Shilingi Bilioni 10.03 sawa na asilimia 28 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010201: Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda**

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kutoa huduma ya kuimarisha sekta ya viwanda. Mafanikio ya utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imeshiriki katika vikao vya kimataifa na kikanda vinavyolenga kuimarisha sekta ya viwanda ikiwemo kushiriki katika kupitia nyaraka za maandalizi ya uandaaji wa Sheria ya (Rules of Origin) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)'. Sambamba na kushiriki katika ziara ya kimataifa ya kutembelea maendeleo ya sekta ya viwanda nchini Indonesia.
i. Wizara kwa kushirikiana na ZIPA imefanya mkutano na wamiliki wa viwanda kwa lengo la kujadili hali ya uzalishaji, masoko, fursa za uwekezaji na changamoto zilizopo pamoja na kushauriana namna bora ya kuzitatua changamoto hizo. Vile vile, Wizara imefanya kikao na Wadau wa Viwanda kujadili mikakati ya pamoja ya kukuza shughuli za uzalishaji na kuongeza thamani katika sekta ya viwanda.
ii. Wizara imefanya uhamasishaji wa viwanda kuhamia katika mitaa ya viwanda ili kupunguza changamoto ya uwekezaji wa viwanda unavyofanywa katika maeneo ya makazi ya watu. Miongoni mwa viwanda vilivyohusishwa katika mazungumzo hayo ni kiwanda cha Zan Paper Industry Limited (Tissue & Toilet Paper) na Tanoma Company Limited (Wipes).
iii. Wizara imefanya ufuatiliaji wa Mradi katika eneo la viwanda Chamanangwe kwa lengo la kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo ambapo kwa sasa umefikia asilimia 42.36.
iv. Wizara imefanya kikao kimoja (1) cha Mpango Shirikishi wa Nchi (PCP) ambacho kimejadili dhana ya Mpango Shirikishi wa nchi kwa maendeleo

endelevu ya viwanda pamoja na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utendaji wake. Kikao hicho kimeshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo UNIDO, Baraza la Biashara Zanzibar (ZNBC), Jumuiya ya Wasafirishaji Nje (ZEXA), Jumuiya ya Wafanya Biashara Zanzibar (ZNCC), Baraza la Wazalishaji Zanzibar (MCZ), “Zanzibar Freight Forward” (ZFB) na Jumuiya ya Wafanyabiashara Wanawake Zanzibar (ZWCC).

v. Wizara imekusanya takwimu za viwanda na kuziingiza katika mfumo wa Viwanda ambapo jumla ya Viwanda 19 vimesajiliwa katika mfumo huo.

**53. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 35.98 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 programu ndogo hii ilipangiwa Shilingi Bilioni 35.90 na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya Shilingi Bilioni 10.03 sawa na asilimia 28 ya fedha zilizopangwa zimeingizwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 9.87 ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo na Shilingi milioni 158.76 kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara.

**SR010202: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali**

**54. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya maendeleo ya Wajasiriamali inatekelezwa na Idara ya Viwanda na ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera ya MSME’s na Uendelezaji wa Wajasiriamali na kuongeza mchango wa uzalishaji wa sekta ya wajasiriamali katika pato la Taifa.

Mafanikio ya utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Japan (JICA) na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Duniani (UNIDO), imetoa mafunzo ya kuongeza ufanisi kwa wajasiriamali 60 Unguja na Pemba, ambapo saba (7) kati yao waliendelea na mafunzo ya vitendo (3 Unguja na 4 Pemba).
ii. Wizara imefanya maadhimisho ya siku ya Kaizen tarehe 13 Januari ambapo wadau mbali mbali wa viwanda wakiwemo wamiliki na wajasiriamali 60 wamehudhuria.

**55. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Milioni 32.01 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 programu hii ilipangiwa Shilingi Milioni 23.27 kwa ajili ya kutekeleza huduma ya Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's . Hadi kufikia Machi, 2026 programu hii haikuingiziwa fedha za matumizi.

**PR0103: Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara**

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inasimamiwa na Idara ya Biashara pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Programu hii ina Programu ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji.

ii. Programu ya Uwezeshaji Biashara.
iii. Programu ya Utengamano wa Kibiashara.

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 17.02 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu hii ilipangiwa Shilingi Bilioni 15.67 na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya Shilingi Bilioni 6.84 sawa na asilimia 44 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010301: Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji**

58. **Mheshimiwa Spi**ka, Programu hii inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko na ina jukumu la kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika usafirishaji wa bidhaa katika masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa pamoja na kuongeza fursa za masoko. Mafanikio ya utekelezaji wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imefanya Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara yaliyojumuisha jumla ya washiriki 316 zikiwemo Taasisi za Serikali 101, Taasisi binafsi 20, na wafanyabiashara/wajasiriamali wa ndani 184. Aidha, washiriki 11 kutoka nchi ya Uganda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Msumbiji, Misri na Brazil wameshiriki katika maonesho hayo.
ii. Wizara imefanikikwa kuimarisha miundombinu ya maji kwa ukarabati wa kisima katika eneo la maonesho pamoja na kuanza hatua ya msingi ya

ujenzi wa eneo la chakula katika eneo la maonesho Dimani.

iii. Wizara imeratibu ushiriki wa wajasiriamali katika maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara (saba saba) kwa lengo la kutoa fursa kwa wajasiriamali wa ndani, kampuni binafsi na taasisi za Serikali kuzitangaza bidhaa na huduma zao ambapo jumla ya washiriki 45 walishiriki kupitia banda la Zanzibar. Kupitia maonesho hayo wajariamali wameweza kupata makubaliano ya kibiashara na wafanyabiashara baada ya kumalizika kwa maonesho. Aidha, Wizara ilishiriki katika Maonesho ya kilimo (Nane nane) yaliyofanyika Dole.

59. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 11.13 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) programu ndogo hii ilipangiwa Shilingi Bilioni 10.97. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya Shilingi Bilioni 2.97 sawa na asilimia 27 ziliingizwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 2.79 ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo na Shilingi Milioni 177.78 zimeingizwa kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara.

**SR010302: Programu Ndogo ya Uwezeshaji Biashara**

60. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Biashara pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara zinazopokea Ruzuku zikiwemo Tume ya Ushindani Halali wa Biashara, Wakala wa Vipimo, Mamlaka ya Usimamizi na Utoaji wa Leseni, Baraza la Taifa la Biashara, Baraza

la Ushindani Halali wa Biashara na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ambazo zina jukumu la kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo: -

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Idara ya Biashara na Ukuzaji masoko imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo kupitia Programu ndogo hii:-

   i. Wizara imefanya ukaguzi katika maeneo ya biashara 89 na kutoa hati za usajili wa biashara 157 kwa wafanyabiashara, kati ya hizo hati 89 ni mpya na 68 wameongezewa muda. Aidha, Wizara imeendelea kutoa vibali vya usafirishaji wa mizigo na kufikia vibali 288 ambapo bidhaa zilizosafirishwa kwa kipindi hicho ni bidhaa chakavu, mazao ya baharini na makapi ya ngano.

   ii. Wizara imefanya kikao na wafanyabiashara waliopewa kibali cha kuingiza bidhaa ya Sukari nchini. Lengo la kikao hicho ni kujadili mwenendo wa uingiaji wa sukari nchini na ununuzi wa sukari inayozalishwa na Kiwanda cha Sukari Mahonda. Aidha, kikao na Wafanyabiashara wanaosafirisha Chuma Chakavu kimefanyika kwa lengo la kupeana uelewa wa changamoto zinazojitokeza za wizi wa Transfoma na nyaya za umeme ambazo huharibu miundombinu ya umeme.

   iii. Wizara imefanya ukaguzi katika masoko ya Zanzibar kwa kuangalia mwenendo wa bei za bidhaa nchini hasa kwa bidhaa muhimu za chakula (Mchele

unga wa ngano, mafuta ya kupikia na sukari). Aidha, ukaguzi katika maghala ya wafanyabiashara wakubwa wanaoingiza bidhaa nchini kwa lengo la kuangalia hali ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula nchini maghalani hufanyika kila wiki.

iv. Wizara imetoa vibali vya kusafirisha bidhaa mbali mbali kwenda nje ya Nchi ikiwemo China, Italy, India, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Comoro, Marekani, Belgium, Denmark, Kenya, Oman, Ufaransa, Malaysia, Bangladesh. Bidhaa hizo ni Mazao ya Baharini, Viungo, Matunda, Nafaka, Vipuri vya ndege, Bidhaa chakavu na Vitenge. Aidha, bidhaa zilizosafirishwa kupelekwa Tanzania Bara ni pamoja na bidhaa chakavu na mafuta ya kula.

62. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Taasisi zinazopokea Ruzuku kupitia programu hii ndogo zimefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

**a) Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara (BLRA)**

63. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti Utoaji wa Leseni ina jukumu la kusimamia na kudhibiti mifumo ya utoaji leseni, tozo na ada za leseni, vibali na ruhusa za ufanyaji biashara kwa Mamlaka za Utoaji Leseni na vibali vya Biashara ndani ya visiwa vya Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Mamlaka imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Wizara imefanya Tathmini ya Mazingira Wezeshi ya Ufanyaji biashara (Zanzibar Business Enabling Environment 2025) kwa kuzingatia vigezo 13 kati ya hivyo vigezo 10 vinatumiwa na Benki ya Dunia na vigezo vitatu (3) vimetumika kulingana na mazingira ya biashara ya Zanzibar.
ii. Vikao na Taasisi 13 vimefanyika kwa lengo la kuunganisha baadhi ya ada na tozo za Maduka ya dawa na biashara za hoteli za kitalii.
iii. Vikao vinne (4) vya uhakiki wa taarifa za leseni na Mfumo wa utoaji leseni vimefanyika na taarifa hizo zimeingizwa katika daftari.
iv. Ukaguzi kwa Taasisi 57 za utoaji leseni, vibali na ruhusa za ufanyaji biashara umefanyika kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa miongozo na kuangalia changamoto zinazojitokeza.
v. Rasimu ya Kanuni kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza imeandaliwa sambamba na kutoa mafunzo ya Sheria ya Mwaka 2025 ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara Pemba.

**b)Baraza la Taifa la Biashara ( ZNBC)**

**64.** **Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Biashara lina jukumu la kukuza mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi, kuweka utaratibu wa majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuyapitia mambo yanayotokana na mikutano au majadiliano ya Jukwaa yanayohusiana na maendeleo ya kiuchumi na

kushauri njia sahihi za utatuzi. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Baraza limefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Uratibu wa Majukwaa ya majadiliano (PPD) vimefanyika kwa kufanya mikutano ya Mabaraza ya Mikoa, na Kamati Tendaji ambayo yaliwezesha kufanyika kwa majadiliano ya Sera, utatuzi wa changamoto za biashara na ufuatiliaji wa maamuzi.
ii. Vikao maalum (Breakfast meetings) vilifanyika kwa kuwakutanisha Taasisi za Serikali na Sekta binafsi ili kujadili changamoto za Viwanda, Wazalishaji wa mwani, Watoa huduma za mitandao na masuala ya Haki Miliki na urahisi wa kufanya biashara.
iii. Baraza limeshiriki katika mikutano ya Kamati ya Kitaifa ya Urahisishaji Biashara (NCTF) na vikao vya mradi wa Mark Up II kwa kubadilishana uzoefu na kuimarisha mchango wa Zanzibar katika mageuzi ya biashara.
iv. Jumla ya wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali za kitaalamu, na mfanyakazi mmoja (1) anaendelea na masomo ya Shahada ya Uzamivu (PhD).

### c) Afisi ya Msajili wa Hakimiki (COSOZA)

65. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ina jukumu la kusajili, kukusanya na kugawa mirabaha kwa wamiliki husika wa hakimiliki waliosajiliwa, kuinua kiwango cha wabunifu na wasanii kitaaluma ili wazalishe kazi zitakazokidhi mahitaji ya soko la ndani, kikanda na

kimataifa na kuwezesha mchango wa tasnia hii kubainika katika Uchumi wa nchi. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Afisi imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mafunzo kwa Majaji na Mahakimu 50 wa Mahkama Kuu Zanzibar yametolewa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa Mahakama katika kutoa maamuzi na kusimamia utekelezaji wa haki za Miliki Bunifu. Aidha, Wasimamizi wa Sheria 50 wamepatiwa mafunzo kwa lengo la kuimarisha uwezo wa usimamizi wa Miliki Bunifu Zanzibar.
ii. Hakimiliki 257 zimesajiliwa na Wamiliki wapya 11 wa hakimiliki wamesajiliwa katika kazi za sanaa na ubunifu.
iii. Wabunifu wakongwe 25 (Unguja 15 na Pemba 10) wamefikiwa katika maeneo yao na kupatiwa kiasi cha fedha kinachotokana na eneo maalum la mirabaha kama mafao. Aidha, mgao wa 12 wa Mirabaha umefanyika ambapo wafanyabiashara ya hakimiliki 1,338 wamefaidika na mgao huo.
iv. Operesheni maalumu ya kuangalia uhalali wa biashara kwa maeneo 261 sawa na asilimia 92.8 kati ya maeneo 281 yaliyopangwa umefanyika katika maeneo ya Hoteli (199), Kumbi za Burudani saba (7), Video Libraries (47), Vyuo vikuu vinne (4) na vituo vinne (4) vya Utangazaji. Matokeo ya ukaguzi huo yamesababisha wamiliki wa biashara hizo wasiokua na leseni kukata leseni ya Hakimiliki.
v. Leseni 125 kwa Watumiaji wa hakimiliki zimetolewa, zikiwemo Hoteli 89, Vituo Vya Utangazaji 4 , Kumbi

za Burudani 7 na Maduka ya kukodisha Vinasa sauti na picha 25 ili kusimamia matumizi halali ya kazi za hakimiliki kibiashara.

vi. Uelewa juu ya Miliki Bunifu, umetolewa kwa Taasisi ya Ubunifu ya Nyota Technical Hub na wanachama wa Chama cha Filamu Zanzibar. Vile vile, uelewa juu ya Usimamizi wa hakimiliki pamoja na Leseni za Hakimiliki umetolewa kwa wadau 70 kwa Upande wa Pemba na Vipindi 6 kupitia TV na Redio vimeandaliwa.

vii. Kikao na wadau wa Miliki Bunifu kimefanyika kwa taasisi za Serikali na Binafsi kwa lengo la kujadili na kuanzisha mfumo wa pamoja wa usimamizi na uratibu wa mapambano dhidi ya uharamia wa hakimiliki na bidhaa bandia.

viii. Kikao cha mashirikiano kati ya COSOZA na COSOTA kimefanyika kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi na kubadilishana uzoefu katika masuala ya kiutendaji. Mfanyakazi mmoja (1) amepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mmoja (1) mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo katika utoaji wa huduma za Afisi.

### d) Tume ya Ushindani Halali wa Biashara (ZFCC)

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ushindani Halali wa Biashara ina jukumu la kuimarisha Ustawi wa wananchi wa Zanzibar kwa kushajihisha, kulinda na kuimarisha Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji wa bidhaa na Huduma kwa kuhakikisha kwamba Wafanyabiashara, Wawekezaji,

wenye Viwanda na Wajasiriamali wanafanya shughuli zao bila ya kukwazana katika soko la Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Tume imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ukaguzi wa bidhaa za Vyakula umefanyika ambapo jumla ya Maduka 1,062, Maghala 65 na Supermarket 65 zimekaguliwa. Katika ukaguzi huo, bidhaa tani 26.8 zisizo salama zimepatikana kati ya hizo, tani 3.5 za bidhaa mchanganyiko, tani 2.3 unga wa sembe na tani 21 mchele. Tani 25.3 tayari zimeshateketezwa na tani 1.5 zinasubiri hatua za kisheria zikamilike.
ii. Ukaguzi wa bei elekezi kwa bidhaa zinazodhibitiwa umefanyika na Wafanyabiashara 45 wamepatikana na makosa ya kutoweka bei za utambulisho wa bidhaa. Aidha, Wafanyabiashara 125 wamepatiwa uelewa wa kuweka bei elekezi.
iii. Jumla ya maombi mawili (2) ya Miungano ya Makampuni yameidhinishwa na kikao cha kusikiliza maombi manne(4) ya Miungano ya Makampuni vimefanyika.
iv. Uwepo wa Makampuni saba (7) yaliyoungana bila kuwasilisha taarifa zao Tume umebainika na hatua za kuwajulisha BPRA na TRA ili kuwapatiwa taarifa Tume juu ya hisa za zamani na za sasa umefanyika kwa Kampuni hizo.
v. Uchunguzi wa bidhaa ya Mafuta ya kupikia umefanyika na kubaini uwepo wa upangaji wa bei kinyume na taratibu. Kupitia ukaguzi huo Wafanya biashara wamepatiwa mafunzo kwa lengo la kuwakumbusha juu ya makosa yaliyobainika na

kuwapa uelewa wa Sheria ya Ushindani Halali wa biashara Namba 5 ya mwaka 2018.

vi. Jumla ya Mikataba (25) ya Huduma za upande mmoja imekaguliwa kwa lengo la kuondoa vigezo na masharti kandamizi na kutakiwa kulipa ada ya usajili.

vii. Uwelewa kwa Wajasiriamali 300, Wafanyabiashara 60 na Maafisa 20 wa Baraza la Mji Kaskazini (A) umetolewa juu ya bei elekezi na bidhaa bandia. Uelewa kwa Wafanyakazi wa Serikali 25 umetolewa juu ya utambuzi na udhibiti wa Bidhaa Bandia aina ya Kiwi, iphone na dawa za matumizi ya binaadamu. Aidha, watendaji saba (7) wa Tume wamepatiwa uelewa juu ya kuzitambua bidhaa bandia za mashine ya boti zenye alama ya biashara ya Yamaha Motor.

**e) Wakala Wa Vipimo (ZAWEMA)**

**67. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa vipimo ina majukumu ya kusimamia maswala yote yanayohusiana na Vipimo hapa Zanzibar, ikiwa ni kuvihakiki vipimo hivyo pamoja na kuhakikisha kwamba Vipimo vyote vinavyotumika kibiashara vinatumika katika utaratibu unaotakiwa kisheria bila ya kuathiri maslahi ya Muuzaji au Mnunuzi. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026 Wakala umefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mizani 1,659, mita za mafuta 592, magari ya kusambazia mafuta vituoni 60, matangi ya mafuta 56, gesi ya matumizi ya nyumbani tani 11, 275.06, mita za bohari na mita za uwanja wa ndege 60

na bidhaa zilizofungashwa kwa viwanda vinne (4) zimehakikiwa. Aidha, lita za mafuta 242,763,093 kutoka nje ya nchi zimehakikiwa.

ii. Rasimu ya Mkataba wa huduma pamoja na Kanuni za bidhaa zilizofungashwa zimeandaliwa.

**f) Baraza la Ushindani Halali wa Biashara (ZFCT)**

68. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lina jukumu kuu la kusimamia haki kwa ngazi ya rufaa katika masuala yanayohusu ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji wa bidhaa na huduma Zanzibar.Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Baraza limefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuandaa Rasimu ya marekebisho madogo ya Sheria ya Ushindani Halali na Kumlinda Mtumiaji nambari 5 ya mwaka 2018, kuandaa Miundo ya Utumishi ya Baraza pamoja na kuandaa andiko la vihatarishi vya Baraza kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Baraza.

ii. Uimarishaji wa Mfumo wa uwasilishaji Mashauri ya Rufaa kwa Baraza (TAMS) umefanyika kwa kuongeza muda wa kibali na matumizi ili kuweza kusomana na mifumo ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa Tanzania.

iii. Wawekezaji 14 kutoka Pemba na Wawekezaji 20 kwa upande wa Unguja wamejengewa uelewa kuhusu sheria, haki na wajibu wao kwa Baraza, pamoja na matumizi sahihi ya mfumo wa TAMS.

iv. Kongamano linalohusiana na mada ya ‘Lijue

Baraza na Mfumo wa Uwasilishaji Mashauri (TAMS) limeandaliwa kwa kuwashirikisha watendaji kutoka Mamlaka za Udhibiti, Wafanyabiashara, Mahakama, Wajasiriamali na Baraza la Vijana la Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba;

v. Vipindi viwili (2) vya redio na viwili (2) vya Televisheni vimeandaliwa vilivyoeleza uwepo wa Baraza na kazi zake na ushindani halali wa biashara na mazingira bora ya biashara.

vi. Ukarabati wa jengo la Ofisi Kisauni unaendelea ambapo kwa sasa umefikia asilimia 68.20. Aidha, Ofisi inatarajia kuhamia katika jengo hilo ifikapo mwezi Juni 2026.

**69. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Bilioni 5.82 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2025 – Machi, 2026 programu ndogo hii ilipangiwa Shilingi Bilioni 4.66 na hadi kufikia Machi 2026, jumla ya Shilingi Bilioni 3.86 sawa na asilimia 83 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010303: Programu Ndogo ya Utengamano wa Kibiashara**

**70. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha biashara huria ambayo itapelekea kuongezeka kwa masoko na uwekezaji baina ya Zanzibar na Nchi nyengine. Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 ni kama ifuatavyo: -

i. Wizara imeshiriki katika kikao cha kuandaa Rasimu ya Mpango wa Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation Roadmap 2026/2031) na kikao cha kamati ya kuondoa vikwazo vya Biashara visivyo vya kodi (NTBs) kwa lengo la kupokea na kupitia changamoto na vikwazo vilivyopo na kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Wizara ilishiriki katika mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya biashara ya mtandao (e-commerce) ikiwa ni miongoni mwa utekelezaji wa mkakati wa biashara ya mtandao wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kupitia nyenzo (tools) za ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa biashara ya mtandao katika ngazi ya kitaifa.

ii. Wizara imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya kikanda inayohusiana na biashara za kimataifa. Mikutano hiyo ni pamoja na mkutano wa kamati ya Kikanda ya Biashara ya Huduma iliyojadili ajenda mbali mbali zilizolenga kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara ya huduma kwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuinua kipato cha nchi husika na kuongeza ajira, mkutano wa kupitia na kuandaa Kanuni za uasili wa bidhaa (Rules of Origin) na mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (National Committee on Trade Facilitation).

71. **Mheshimiwa Spika,** Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi Milioni 59.78 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2025 – Machi 2026

programu ndogo hii ilipangiwa Shilingi Milioni 45.61 na hadi kufikia Machi 2026, programu hii ndogo haikuingiziwa fedha.

## F. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026.

### F.1.Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)

72. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ZBS ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni 9.677 kwa ajili ya kutekeleza kazi zake kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 6.899 kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi Bilioni 2.777 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026 Shilingi Bilioni 5.404 zilitumika sawa na asilimia 55.84 ya makadirio.

73. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ZBS ilikadiria kukusanya Shilingi Bilioni 9.677 kutokana na vyanzo vyake vya ndani vya mapato na hadi kufikia Machi, 2026 Shilingi Bilioni 9.622 sawa na asilimia 99.44 ya makadirio.

74. **Mheshimiwa Spika,** ZBS kwa mwaka 2025/2026 iliidhinishiwa kuchangia jumla ya Shilingi Bilioni 2.40 katika mfuko wa Hazina. Hadi kufikia Machi, 2026 iliwasilisha mchango wa Shilingi Bilioni 1.80 katika Mfuko wa Hazina sawa na aslimia 75.

**75.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2025/2026 ZBS imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Jumla ya viwango 94 vimeandaliwa na viwango 301 vimeuzwa. Aidha Leseni za matumizi ya Alama ya Ubora 24 kwa kutumia kiwango cha Zanzibar (ZBS Quality Mark) zimetolewa na Vyeti 38 vimehuishwa baada ya kumaliza muda wake; **Kiambatanisho nambari 6.**

ii. Ukaguzi wa bidhaa 613 umefanyika na kupatiwa vyeti vya ubora kupitia mfumo wa ukaguzi nje ya nchi (PvoC). Aidha, ukaguzi wa Kontena 10,755 za Futi (40), Kontena 13,462 za futi (20) kupitia Mfumo wa Destination Inspection (DI) umefanyika. Gari 5,356, pikipiki 13,083 , Mafuta ya Nishati lita 240,862,196 zimehakikiwa kupitia mfumo wa DI.

iii. Ukaguzi wa shehena 7,436 za bidhaa katika Uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar umefanyika . Aidha, jumla ya Kaguzi 45 zilifanyika Masokoni.

iv. Sampuli 2,428 za bidhaa zimepokelewa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara kati ya hizo sampuli za bidhaa 434 hazikukidhi matakwa ya kiwango husika;

v. Taasisi imeshiriki majaribio ya (Proficiency Testing – PT) kwa maabara ya Umeme na Elektroniki, imefanya PT – 2, Vifungashio PT – 1, Nguo na Ngozi PT – 1, Makanika PT – 1, maabara ya Kemikali (Mafuta ya ndege – Jet A1) PT - 1 kwa mujibu wa matakwa ya kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 katika taratibu za kupata ithibati ya maabara hizo.

vi. Watendaji 37 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya kuhamasisha jamii juu ya huduma za ZBS kwa kutumia vyombo vya habari, bonanza na mitandao ya kijamii na kuanza matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Kielektroniki wa Taasisi.

### F.2.Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar (BPRA)

**76. Mheshimiwa Spika,** BPRA kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Bilioni 4.52 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2025 hadi Machi 2026, BPRA ilipanga kutumia Shilingi Bilioni 3.59 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya Shilingi Bilioni 3.04 sawa na asilimia 85 zilitumika. Shilingi Bilioni 1.59 zilitumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni 1.09 zilitumika kwa malipo ya mishahara na Shilingi Milioni 360.0 ziliingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**77. Mheshimiwa Spika,** BPRA kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 5.0 kutoka katika vyanzo mbali mbali kwa huduma zinazotoa. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ilipanga kukusanya Shilingi Bilioni 3.9. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya Shilingi Bilioni 5.702 sawa na asilimia 146 zilimekusanywa.

**78. Mheshimiwa Spika,** BPRA kwa mwaka 2025/2026 iliidhinishiwa kuchangia jumla ya Shilingi milioni 480 katika

mfuko wa Hazina. Hadi kufikia Machi, 2026 iliwasilisha mchango wa Shilingi milioni 360 katika Mfuko wa Hazina sawa na asilimia 75.

79. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 BPRA imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

   i. Mfumo wa usajili wa biashara na mali "Online Registration Service" (ORS) umeboreshwa pamoja na kufanya ununuzi wa "platform" ya huduma kwa wateja na matengenezo ya tovuti. Aidha, warsha ya uwelewa kwa wadau kuhusu utengenezwaji wa Mfumo mpya wa Usajili wa Biashara na Mali imefanyika
   ii. Sheria ya Nyaraka, Majina ya Biashara, Usajili wa Biashara, Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na Sheria ya Umilikishaji wa Biashara kwa Mkataba (Franchise) zimefanyiwa mapitio. Aidha, ukaguzi na Uhakiki wa Kampuni na Majina ya Biashara na Alama za Biashara na Nyaraka katika wilaya ya kusini (Michamvi) na Magharibi B (Uwanja wa ndege) umefanyika.
   iii. Usajili wa Kampuni 1,239, Majina ya Biashara 1,631, Mali Ubunifu (Alama za Biashara) 1,070, na Nyaraka 9952 zimesajiliwa pamoja na kufanya vipindi sita (6) vya kutoa uwelewa kuhusu umuhimu wa usajili wa biashara na Mali.
   iv. Utoaji wa elimu kuhusu utaratibu wa mirathi kwa wasiokuwa waislamu umefanyika. Aidha, faili 26 za mirathi kwa wasiokuwa waisilamu zimefunguliwa na

tayari mirathi 23 washapewa warithi wao.

v. Uhamasishaji wa umuhimu wa usajili wa logo katika biashara umefanyika na mafunzo kwa Masheha kuhusu shughuli zinazofanywa na Wakala yamefanyika kwa Wilaya za Chake Chake, Micheweni na Wete na mafunzo katika vituo vinne (4) vya kukuza ubunifu vya (HUB) Mbweni KIST, Shangani Cube, Al- Sumeit na Statuo Association Hub yamefanyika.

vi. Mfanyakazi mmoja ( 1) amepatiwa mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili fani ya Uongozi wa Tehama na wafanyakazi 20 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali.

### F.3.Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)

80. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Shirika liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika (Corporate Strategic Plan) wa miaka mitatu 2023-2025 pamoja na Mpango wa Biashara wa miaka mitano 2020-2025.

81. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/26 Shirika lilikadiria kutumia jumla ya Shilingi Bilioni 121.50 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za Maendeleo, ambapo Shilingi Bilioni 118.51 zilipangwa kutumiwa kwa kipindi cha miezi tisa. Hadi kufikia Machi, 2026 Shirika limetumia jumla ya Shilingi Bilioni 92.69 sawa na asilimia 78.21 ya makadirio kwa miezi tisa.

82. **Mheshimiwa Spika,** Shirika katika kipindi hiki cha miezi tisa (9) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 lilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 125.79 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vikiwemo; mauzo ya karafuu, mafuta ya mimea na mapato yanayotokana na Majengo. Aidha, Shirika limefanikiwa kuuza karafuu nje ya nchi kwa bei ya Dola za Kimarekani 6,800 kwa tani moja FOB Zanzibar na jumla ya tani 5,463.13 za karafuu zimeuzwa katika kipindi hiki cha miezi tisa. Hadi kufikia Machi 2026 Shirika limeweza kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 92.6 sawa na asilimia 73.5 ya makadirio ya miezi tisa.

83. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026 Shirika limefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Shirika limeweza kununua tani 5616.1 za karafuu kavu kutoka kwa Wakulima kwa gharama ya Shilingi Bilioni 83.9, tani 793.2 za makonyo kwa gharama ya Shilingi Bilioni 1.57 kupitia msimu wa wastani wa vuno la karafuu.

ii. Shirika limezalisha jumla ya lita 1,598.7 za mafuta yatokanayo na mdalasini, mchaichai, mrehani na mkaratusi.

iii. Katika kuimarisha ustawi wa wakulima, Shirika lilisimamia malipo ya bima kwa wakulima 115 walioanguka katika mwaka 2025/2026. Kati ya hao, wakulima 34 wamelipwa jumla ya Shilingi Milioni 38, huku wakulima 81 wakiendelea kufuatiliwa ili kuhakikisha wanapatiwa malipo yao stahiki.

iv. Katika juhudi za kuimarisha uzalishaji wa zao

la karafuu, Shirika limenunua miche 113,531 ya mikarafuu yenye thamani ya Shilingi Milioni 113.53 na kuigawa kwa wakulima Unguja na Pemba. Aidha, Shirika limeendelea kushirikiana na chuo cha mafunzo katika utekelezaji wa utaratibu wa kuanzisha mashamba mapya ya mikarafuu katika maeneo ya Kinumoshi, Machui na Langoni, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuongeza uzalishaji wa muda mrefu.

v. Shirika limeendelea kushirikiana na Kikosi cha Kupambana na Magendo pamoja na wananchi wema katika kukusanya taarifa za usafirishaji haramu wa karafuu, hatua inayolenga kudhibiti upotevu wa zao hilo muhimu kwa uchumi wa Zanzibar.

vi. Shirika limefungua kituo kipya cha ununuzi wa karafuu katika eneo la Kiwani, Pemba, sambamba na kufanya matengenezo makubwa ya vituo saba vya ununuzi wa karafuu. Hatua hii imelenga kuboresha mazingira ya ununuzi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa zao hilo.

vii. Shirika limetoa mafunzo kwa wakulima kuhusu athari za magendo ya karafuu kwa sekta ya karafuu na kwa uchumi wa Zanzibar kwa ujumla, ili kuongeza uelewa na ushiriki wao katika kulinda zao hilo.

### F.4. Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO)

**84. Mheshimiwa Spika,** ZASCO kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeendelea na utekelezaji wa shughuli zake kwa kuzingatia Mpango kazi wake. Katika utekelezaji wa

kazi zake, Kampuni ilikadiria kutumia jumla ya shilingi Bilioni 12.97. Hadi kufikia mwezi Machi, 2026, Kampuni ilitumia Shilingi Bilioni 7.56 sawa na asilimia 58.2 kwa ajili ya kazi za kawaida na mradi wa maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi Bilioni 6.630 kwa ajili ya maendeleo ambapo mitambo ya usarifu wa mwani imenunuliwa na Shilingi milioni 930.7 kwa kazi za kawaida.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2026, Kampuni ya Mwani imetekeleza Progamu zake kama ifuatavyo:

i. Kampuni imekamilisha taratibu za kumpata Mzabuni wa awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha mwani Chamanangwe Pemba.

ii. Kampuni imekamilisha taratibu za kumpata mzabuni wa kusambaza mashine za kusarifu mwani. Kukamilika kwa taratibu hizo kumepelekea kufanikisha malipo kwa Wazabuni wa mitambo ya kuchakata mwani kwa ajili ya Kiwanda cha mwani Chamanangwe Pemba. Mitambo hiyo inatarajiwa kuwasili nchini hivi karibuni.

iii. Kampuni inaendelea na majadiliano ya uwekezaji na Kampuni ya MDAHX kwa ajili ya kuingia katika ushirikiano wa kuanzisha kiwanda cha kusarifu mwani Unguja. Majadiliano hayo yamepelekea kuanzisha Kampuni ya Ubia baina ya ZASCO na MDAHX ambayo inaitwa Mwani Blue kwa ajili ya kusarifu mwani na kutoa mazao mbali mbali ya mwani. Tayari Kampuni hiyo imeshasajiliwa na inatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni.

iv. Katika kuimarisha biashara ya mwani, Kampuni ilifanya jitihada za kutafuta masoko ya mwani na kununua mwani kwa wakulima. Katika kipindi cha miezi tisa, Kampuni imenunua tani 63.5 za mwani. Kati ya hiyo, tani 11.2 ni mwani aina ya Spinosum na tani 52.4 aina ya Cottonii;

v. Kampuni imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Ubora wa Mwani na Uhifadhi kupita Shirika la UNCDF. Mradi huo unaendelea vizuri na utekelezaji wake ambapo shughuli mbali zimekamilika zikiwemo kujenga makaushio ya mwani kwa kutumia jua ambayo yamejengwa katika kijiji cha Jongowe kwa Unguja na Makangale kwa Pemba na kununua boti na mashine kwa ajili ya kurahisisha uchukuzi wa mwani baada ya mavuno ambapo boti tatu (3) za mashine zimenunuliwa. Kati ya boti hizo, mbili (2) zina ukubwa wa mita saba (7) na moja (1) ina mita tano (5). Boti hizo zimeshakabidhiwa kwa wakulima wa mwani wa Shehia ya Makangale kwa Pemba na Tumbatu kwa Unguja;

vi. Kampuni imefanya mazungumzo na Wawekezaji ambao wameonesha nia ya kufanya biashara ya mwani na ZASCO. Wawekezaji hao wanatokea China, Mauritius na Afrika ya Kusini. Katika mazungumzo hayo, Kampuni hutoa taarifa za msingi kuhusu mwani inaozalisha zikiwemo za ubora wa mwani. Aidha, imepeleka sampuli mbali mbali za mwani kwa wateja wanaohitaji kufanya biashara. Sampuli hizo zimepelekwa kwa dhamira ya kuwawezesha wateja hao kujiridhisha kuhusu ubora

wa mwani ambapo jumla ya kilo 549 zimetumwa kwa wateja kutoka nchi za Singapore na Uturuki. Sample hizo ni za mwani wa “Spinosum”, “Cottonii” na “Ulva”;

vii. Kampuni imeshiriki katika maonesho ya kibiashara ya Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Dole Mjini Unguja na maonesho ya Miaka 62 ya Mapinduzi Zanzibar yaliyofanyika Dimani. Kampuni ilipata fursa ya kujitangaza na kuongeza mtandao (networking) kwa wadau mbali mbali wa mwani waliofika katika banda la Kampuni;

viii. Kampuni pia ilifanya kikao pamoja na mahojiano na Kampuni Binafsi ya Solveris Consultancy Limited kutokea Dar es Salaam kwa ajili ya majadiliano ya masuala mbali mbali ya Mwani ikiwa ni pamoja na mnyororo wa thamani, uboreshaji, soko, ujasiriamali, wadau wanaojishughulisha na Mwani pamoja na changamoto za utekelezaji. Lengo la majadiliano hayo ni kupata taarifa zitakazosaidia katika utafiti unaofanywa na taasisi hiyo kuhusu masuala mbali mbali ya Mwani; na

ix. Huduma za uendeshaji wa ofisi zimeendelea kuimarishwa ikiwemo huduma ya ulinzi, ununuzi wa kompyuta, printa, makabati, umeme, mafuta ya gari na vifaa vya usafi na kuweka mazingira mazuri ya kiutendaji.

## G. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE KWA IDARA NA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### G.1. Vipaumbele vya Idara na Taasisi Zinazopokea Ruzuku kwa Mwaka 2026/2027

86. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia fungu 017 imepanga kutekeleza vipaumbele kupitia programu kuu tatu (3) katika kutekeleza maeneo makuu matatu (3) ambayo yanalenga kuimarisha Sekta ya viwanda, kuimarisha Biashara na kutafuta Masoko pamoja na kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na utoaji huduma. Maeneo hayo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kama ifuatavyo:-

### G.2. Sekta ya Viwanda

87. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza sekta ya viwanda, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

   i. Kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda Dunga Zuze na Chamanangwe kwa Ujenzi wa majengo ya viwanda vidogo na vya kati, Unguja majengo manne (4) na Pemba majengo mawili (2).
   ii. Ujenzi wa uzio kuzunguka maeneo ya viwanda Dunga zuze na Chamanangwe.
   iii. Ujenzi wa Barabara katika maeneo ya viwanda Chamanangwe.

iv. Kuendeleza ujenzi wa tangi la maji katika eneo la viwanda Chamanangwe.

**G.3.Sekta ya Biashara**

88.**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Biashara, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuendeleza Ujenzi kwenye eneo la maonesho ya kibiashara Dimani kwa ujenzi wa ukumbi wa matukio wakati wa maonesho  na Ujenzi wa kumbi za maonesho.

ii. Ujenzi wa mkahawa katika eneo la maonesho. Aidha, Wizara itaendelea uratibu wa uandaaji wa Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (MICE) chini ya ufadhili wa Korea Exim Bank.

**G.4.Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma**

89. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Mazingira ya ufanyaji Biashara, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuandaa Mkakati wa Urasimishaji Biashara pamoja na Muongozo wake.

ii. Kufanya mapitio ya Sheria ya Biashara ya mwaka 2013 na Kanuni zake ikiwemo Kanuni ya Vyuma Chakavu, Sheria ya Leseni ya mwaka 1983, Kanuni za Sheria nambari 1 ya mwaka 2025 na Sheria ya Hakimiliki (Namba 14) ya mwaka 2003.

iii. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara, Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara na Mpango Mkakati wa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki.
iv. Kuanzisha mfumo wa Udhibiti wa Bidhaa Bandia.
v. Kuunganisha Mfumo wa TAMS na Mfumo wa Mahkama Kuu na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania.
vi. Kufanya tafiti za malighafi zinazopatikana Zanzibar kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa Viwanda vya ndani na tafiti za bidhaa zinazotumiwa na wageni, kutathmini uwezo wa uzalishaji, mahitaji na masoko.

## H. VIPAUMBELE KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027

90. **Mheshimiwa Spika**, Vipaumbele kwa taasisi zinazojitegemea kwa mwaka 2026/2027 ni kama ifuatavyo:-

### H.1. Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA)

91. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-
i. Kuimarisha na kutengeneza mifumo ya Usajili wa Mali na Biashara kwa lengo la kuongeza ufanisi wa usajili na kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara.
ii. Kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali, kwa lengo la kuongeza urasimishaji wa biashara na kuchochea ukuaji wa uchumi.

iii. Kuimarisha ushirikiano wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na Taasisi nyengine kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara kwa ujumla na kubadilishana taarifa za biashara.

**H.2.Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)**

92. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza Taasisi ya Viwango, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Uendelezaji wa Maabara za Kemikali, Chakula, Uhandisi Ujenzi,Uhandisi Mitambo, Umeme na Elektroniki na Metrolojia – Mass.

ii. Kuweka mfumo wa iSQMT na Digital katika Taasisi utakaofanikisha mifumo katika kurahisisha utekelezaji wa utoaji wa Huduma wa kazi za Taasisi.

iii. Kupata Ithibati (Accreditation) ya Maabara tano (5) na Ithibati ya Kituo cha Ukaguzi wa Vyombo vya moto kwa kutumia kiwango cha ISO 17020:2012.

iv. Ujenzi wa Ofisi na Maabara Chamanangwe Pemba na Ujenzi wa jengo la Upimaji (Test House) eneo la Viwanda Dunga.

**H.3.Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)**

93. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Biashara la Taifa itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Shirika linatarajia kuuza kiasi cha tani 2,964 kwa wastani wa bei ya Dola za Kimarekani 7,200 kwa tani moja.

ii. Shirika linatarajia kununua tani 600 za makonyo

makavu kwa wastani wa bei ya Shilingi 2,000 kwa kilo.

iii. Shirika linatarajia kuzalisha mafuta ya mimea ya aina mbali mbali.

iv. Kufanya ujenzi wa maghala kwa ajili ya ukodishaji.

## I. MWELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027

94. **Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, naliomba Baraza lako kuidhinisha mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Fungu 017 kama ifuatavyo;-

### I.1. Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

95. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 3.00. Ninaomba Baraza lako kuidhinisha Mapato ya Shilingi Bilioni 3.00 Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio kama inavyoonekana katika **Kiambatanisho nambari 4.**

### I.2. Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

96. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2026/27 imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni 49.95 Kati ya fedha hizo

Shilingi Bilioni 2.94 kwa Matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi Bilioni 3.26 kwa malipo ya mishahara. Shilingi Bilioni 34.26 zimetengwa kwa kazi za Maendeleo. Shilingi Bilioni 9.48 zimetengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara na kazi za kawaida kwa Taasisi za Wizara. **Kiambatanisho nambari 5**

**97.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda itatekeleza Programu Kuu tatu (3). Programu kuu hizo ni (i) Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; (ii) Programu ya Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali; na (iii) Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya kwanza ni Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ambayo imegawika katika Programu ndogo tatu (3). Programu hizo ni (i) Utawala na Uendesheaji wa shughuli za Wizara,(ii) Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti na (iii) Uratibu wa Shughuli za Wizara kwa Pemba.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu Kuu hii iweze kutekeleza shughuli zake naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 4.63.

i. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara iweze kutekeleza shughuli zake, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 3.21.

ii. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara iweze kutekeleza

shughuli zake, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Milioni 602.90.

iii. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba iweze kutekeleza shughuli zake, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Milioni 817.73.

100. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Pili ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali ambayo imegawika katika Programu ndogo mbili. (i) Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda na (ii) Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali.

101. **Mheshimiwa Spika,** Ili Programu hii Kuu iweze kutekeleza shughuli ilizojipangia naomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya shilingi Shilingi Bilioni 26.33.

i. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda iweze kutekeleza shughuli zake naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 26.23

ii. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali iweze kutekeleza shughuli zake naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya Shilingi Milioni 103.8.

102. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya tatu ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara ambayo imegawika katika Programu ndogo tatu (3) (i) Ukuzaji masoko na usafirishaji; (ii) Uwezeshaji biashara na (iii) Utengamano wa Kibiashara. Ili Programu hii Kuu iweze kutekeleza majukumu yake

naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 18.98.

i. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji iweze kutekeleza shughuli zake naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya shughuli ya Shilingi Bilioni 9.28.
ii. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara iweze kutekeleza shughuli zake naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 9.65.
iii. Mheshimiwa Spika, Ili Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara iweze kutekeleza shughuli zake naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Milioni 44.51.

**J. SHUKRANI:**

**103. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2025/2026 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa iliyopatiwa Wizara kutoka kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau hao kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo; Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), EXIM Bank Korea, Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Miliki Bunifu Ulimwenguni (WIPO), TradeMark Africa (TMA), Shirika la Biashara Duniani (WTO), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Jumuiya za Wafanyabiashara, Zanzibar (ZNCC), Wafanyabiashara na Wawekezaji wa

Viwanda wote wakubwa na wadogo, Kampuni ya Yas, Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).

104. **Mheshimiwa Spika,** Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali. Ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya.

105. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda niwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda nikianza na Katibu Mkuu Dkt. Habiba Hassan Omar, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Said Seif Mzee, Wakuu wa Taasisi wote, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa mashirikiano yao wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ni matarajio yangu kwamba mashirikiano hayo yataendelezwa kwa ufanisi zaidi katika mwaka wa fedha 2026/2027 ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

## K. HITIMISHO

106. **Mheshimiwa Spika,** Ili Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda iweze kutekeleza malengo yake naliomba

Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 49.95. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 2.94 kwa Matumizi ya kazi za kawaida, Shilingi Bilioni 3.26 kwa malipo ya mishahara na Shilingi Bilioni 34.26 kwa kazi za Maendeleo. Aidha, Shilingi Bilioni 9.48 kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara na kazi za kawaida kwa Taasisi za Wizara.

107. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaliomba Baraza lako kuidhinisha Mapato ya Shilingi Bilioni 3.00 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

108. **Mheshimiwa Spika** na Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.



**SHARIFF ALI SHARIFF.**
**KAIMU WAZIRI,**
**WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA,**
**ZANZIBAR.**

## L. VIAMBATANISHO

***Kiambatanisho Nambari 1: Mchanganuo wa Fedha zilizopangwa na zilizotumika Julai 2025 hadi Machi 2026***

| Aina ya Fedha | Fedha Zilizopangwa Kwa Mwaka | Fedha zilizopangwa kwa (Julai-Machi) | Fedha zilzizopatikana (Julai-Machi) | Asilimia ya Zilizopatikana |
|---|---|---|---|---|
| Mshahara | 3,475,100,000 | 2,614,725,401 | 2,546,962,740 | 97% |
| Matumizi ya Kawaida | 1,963,250,000 | 1,605,133,800 | 674,348,762 | 42% |
| Ruzuku ya Matumizi | 3,295,800,000 | 2,753,216,405 | 1,518,377,915 | 55% |
| Ruzuku ya Mshahara | 2,456,300,000 | 1,842,300,000 | 2,148,417,974 | 117% |
| Maendeleo | 46,363,870,050 | 46,313,870,050 | 12,669,633,878 | 27% |
| **Jumla Kuu** | **57,554,320,050** | **55,129,245,656** | **19,557,741,269** | **35%** |

*Kiambatanisho Nambari 2: Mchanganuo wa Matumizi kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026*

| Fungu | Programu Kuu/Programu Ndogo | Kiasi Kilichopangwa kwa Mwaka 2024/2025 | Makadirio kwa (Julai-Machi) 2024/25 | Matumizi kwa (Julai-Machi) 2024-2025 | Asilimia | Kiasi kilichopangwa kwa Mwaka 2025/2026 | Makadirio kwa (Julai-Machi) 2025/26 | Matumizi kwa (Julai-Machi) 2025/26 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biasharara na Maendeleo ya Viwanda** | **3,863,419,798** | **2,985,823,123** | **2,505,994,343** | **84%** | **4,520,419,110** | **3,523,389,810** | **2,683,032,601** | **76%** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 2,237,335,998 | 1,715,135,273 | 1,630,126,189 | 95% | 2,956,524,031 | 2,321,499,750 | 1,985,651,339 | 86% |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 522,766,900 | 414,709,175 | 621,216,701 | 150% | 482,519,880 | 379,552,410 | 256,965,189 | 68% |
| SR010103 | Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 1,103,316,900 | 855,978,675 | 254,651,453 | 30% | 1,081,375,199 | 822,337,650 | 440,416,073 | 54% |
| | | | | | | | | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **40,759,520,776** | **40,654,035,582** | **1,245,812,055** | **28%** | **36,012,783,990** | **5,926,679,541** | **0,032,952,543** | **28%** |
| SR010201 | Ukuzaji Viwanda | 40,725,968,776 | 40,631,608,582 | 11,245,812,055 | 28% | 35,980,769,670 | 35,903,405,121 | 10,032,952,543 | 28% |
| SR010202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 33,552,000 | 22,427,000 | - | - | 32,014,320 | 23,274,420 | - | - |
| | | | | | | | | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **15,658,059,426** | **14,390,867,562** | **4,655,466,026** | **32%** | **17,021,116,950** | **15,679,176,305** | **6,841,756,125** | **44%** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 10,368,346,426 | 10,244,696,562 | 1,840,821,346 | 18% | 11,137,729,450 | 10,972,592,400 | 2,973,228,948 | 27% |
| SR010305 | Uwezeshaji Biashara | 5,245,873,000 | 4,113,651,000 | 2,805,619,680 | 68% | 5,823,607,500 | 4,660,973,905 | 3,868,527,177 | 83% |
| SR010306 | Utengamano wa Kibiashara | 43,840,000 | 32,520,000 | 9,025,000 | 28% | 59,780,000 | 45,610,000 | - | - |
| **JUMLA YA KIFUNGU RO1** | | **60,281,000,000** | **58,030,726,267** | **18,407,272,424** | **32%** | **57,554,320,050** | **55,129,245,656** | **19,557,741,269** | **35%** |

***Kiambatanisho Nambari 3: Mapato ya Wizara kwa kipindi cha Miezi Tisa Mwaka wa Fedha 2025/2026***

| Kifungu | Maelezo | Makadirio kwa Miezi Tisa 2024/25 | Makusanyo kwa Miezi Tisa 2024/25 | Asilimia ya Makusanyo kwa Miezi Tisa | Makadirio kwa Mwaka 2025/26 | Makadirio kwa Miezi Tisa 2025/26 | Makusanyo kwa Miezi Tisa 2025/26 | Asilimia ya Makusanyo kwa Miezi Tisa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **441,557,000** | **249,473,271** | **56%** | **1,025,437,000** | **733,520,000** | **331,580,699** | **45%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo (U) | 441,557,000 | 249,473,271 | 56% | 1,025,437,000 | 733,520,000 | 331,580,699 | 45% |
| | | | | | | | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **710,000,000** | **689,801,000** | **97%** | **1,741,788,000** | **1,420,000,000** | **524,653,333** | **37%** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 710,000,000 | 689,801,000 | 97% | 1,741,788,000 | 1,420,000,000 | 524,653,333 | 37% |
| | | | | | | | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **14,000,000** | **19,543,473** | **140%** | **43,636,000** | **39,091,000** | **26,884,720** | **69%** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 14,000,000 | 19,543,473 | 140% | 43,636,000 | 39,091,000 | 26,884,720 | 69% |
| | | | | | | | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRC)** | **48,000,000** | **5,048,728** | **11%** | **91,162,000** | **81,000,000** | **-** | **0%** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa Mamlaka za Leseni | 48,000,000 | 5,048,728 | **11%** | 91,162,000 | 81,000,000 | - | 0% |
| | | | | | | | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **72,247,000** | **62,170,000** | **86%** | **181,693,000** | **164,193,000** | **106,569,098** | **65%** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 72,247,000 | **72,247,000** | **86%** | 181,693,000 | 164,193,000 | 106,569,098 | 65% |
| | | | | | | | | |
| **R0114** | **Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki** | **180,000,000** | **151,317,000** | **84%** | **363,743,000** | **327,267,000** | **227,313,402** | **69%** |
| 1422117 | Mapato ya usajili na Ada | 180,000,000 | 151,317,000 | **84%** | 363,743,000 | 327,267,000 | 227,313,402 | 69% |

| Kifungu | Maelezo | Makadirio kwa Miezi Tisa 2024/25 | Makusanyo kwa Miezi Tisa 2024/25 | Asilimia ya Makusanyo kwa Miezi Tisa | Makadirio kwa Mwaka 2025/26 | Makadirio kwa Miezi Tisa 2025/26 | Makusanyo kwa Miezi Tisa 2025/26 | Asilimia ya Makusanyo kwa Miezi Tisa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ya Mwaka | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **37,448,500** | **32,807,000** | **81%** | **72,208,000** | **58,704,000** | **46,558,531** | **79%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo (P) | 32,807,000 | 27,658,691 | 84% | 72,208,000 | 58,704,000 | 46,558,531 | 79% |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Biashara | 7,500,000 | 4,900,000 | 65% | | | | |
| **Jumla Kuu** | | **1,506,111,000** | **1,209,912,563** | **80%** | **3,519,667,000** | **2,823,775,000** | **1,263,559,783** | **45%** |

***Kiambatanisho Nambari 4: Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026-2027***

| Taasisi | Kasma | Chanzo cha Mapato | Makadirio ya Mapato 2026/27 |
|---|---|---|---|
| ZAWEMA | 14210121 | Mapato kutoka huduma za Vipimo (U) | 820,395,000 |
| PEMBA | 14210121 | Mapato kutoka huduma za Vipimo (P) | 131,172,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **951,567,000** |
| ZFCC | 14220139 | Ada za Mikataba | 1,049,372,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **1,049,372,000** |
| DAP | 14150113 | Mapato ya Ukodishaji | 36,728,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **36,728,000** |
| BLRA | 14220257 | Ada za Udhibiti | 90,999,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **90,999,000** |
| DTM | 14220258 | Ada za Vibalii | 118,084,000 |
| DTM | 14150113 | Mapato ya Ukodishaji | 389,480,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **507,564,000** |
| COSOZA | 14220151 | Ada za Usimamizi na Wakala | 363,770,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **363,770,000** |
| **Jumla Kuu** | | | **3,000,000,000** |

***Kiambatanisho Nambari 5: Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027***

| Fungu | Programu Kuu/Programu Ndogo | Kiasi kilichopangwa kwa Mwaka 2026/2027 |
|---|---|---|
| **P01** | **Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biasharara na Maendeleo ya Viwanda** | **4,638,311,100** |
| S0101 | Utawala na Uendeshaji | **3,217,681,100** |
| S0102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | **602,900,000** |
| S0103 | Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | **817,730,000** |
| | | |
| **P02** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **26,335,822,000** |
| S0201 | Ukuzaji Viwanda | 26,232,022,000 |
| S0202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 103,800,000 |
| | | |
| **P03** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **18,985,736,900** |
| S0301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | **9,289,680,900** |
| S0302 | Uwezeshaji Biashara | 9,651,546,000 |
| S0303 | Utengamano wa Kibiashara | 44,510,000 |
| **JUMLA YA KIFUNGU 017** | | **49,959,870,000** |

***Kiambatanisho Nambari 6: Viwango vya ZBS viliondaliwa na kuuzwa kwa kipindi cha Julai- Machi,2026***

| S/N | AINA YA VIWANGO VILIVYOANDALIW | AINA YA RASIMU | VIWANGO VILIVYOUZWA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI,2026 |
|---|---|---|---|
| 1. | Viwango vya bidhaa za nguo na ngozi | 20 | Viwango vya Chakula |
| 2. | Viwango vya Samaki na bidhaa za baharini | 7 | Viwango vya Kemikali |
| 3. | Uhandisi mitambo na vyombo vya moto | 5 | Viwango vya Mazingira |
| 4. | Umeme na Elektroniki | 11 | Viwango vya Uhandisi Ujenzi |
| 5. | Viwango vya bidhaa za kemikali | 4 | Viwango vya Uhandisi Mitambo |
| 6. | Viwango vya Vifaa vya Ujenzi | 3 | Viwango vya Uhandisi Umeme ; |
| 7. | Viwango vya Vifungashio | 8 | Viwango vya Chakula |
| 8. | Viwango vya Chakula | 12 | |
| 9. | Viwango vya Dawa asili | 3 | |
| 10. | Viwango vya Uhandisi mitambo na vyombo vya moto | 7 | |
| 11. | Viwango vya vyakula vya wanyama | 6 | |
| 12. | Viwango vya Ubora wa maji | 2 | |
| 13. | Viwango vya viungo vya mimea | 4 | |
| 14. | Kikundi kazi cha mwani | 1 | |
| 15. | Kikundi kazi cha ubuyu | 1 | |